# ARDHI YETU

*#Itunze Ikutunze*

Toleo Maalum • Desemba 2024 • Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi

# WIKI YA ARDHI



# VIONGOZI WA WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI



**MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI**
**WAZIRI**



**MHE. GEOPHREY M. PINDA**
**NAIBU WAZIRI**





**MHANDISI ANTHONY D. SANGA**
**KATIBU MKUU**

**LUCY D. KABYEMERA**
**NAIBU KATIBU MKUU**

# Salamu kutoka kwa Waziri wa Ardhi



Nina kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujaalia uhai na uzima wa kuendesha gurudumu la Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi tukiwa wazima wa afya.

Lakini pia sifa nizipeleke kwa Muumba wetu kuniwezesha mimi na watumishi wote wa Wizara ya Ardhi, Nyumba Maendeleo ya Makazi kutekeleza majukumu yetu kwa uaminifu na uadilifu mkubwa.

Wizara hii imeendelea kuwa kiungo wezeshi kwa shughuli za uzalishaji ikiwemo kilimo, viwanda, mifugo, maliasili, utalii, madini na miundombinu ambapo matumizi ya ardhi na uhitaji wake katika sekta hizo ni mkubwa.

Kwa sasa Wizara ya Ardhi iko kwenye mageuzi makubwa ya kubadilisha mifumo yake kutoka analogia kwenda digitali ambapo wizara imeanza kutumia mfumo wa e-ardhi lengo likiwa kuondoa migogoro ya ardhi na wakati huo kuiwezesha serikali kukusanya mapato mengi kupitia sekta hii.

Tukumbuke kuwa, kwa sasa matumizi ya teknolojia siyo hiari tena kwa kuwa, kupitia mfumo wa e-ardhi huduma za sekta ya ardhi zinaboreshwa ili kuwafikia wananchi wengi wakiwemo wale wa vijijini.

Mfumo huu wa e-Ardhi tayari umeanza kutumika kwa baadhi ya maeneo nchini kama vile Dodoma, Arusha, Tabora katika halmashauri ya Nzega, Pwani halmashauri ya Chalinze pamoja na manispaa ya Shinyanga na Kahama zilizopo mkoa wa Shinyanga.

Kupitia mabadiliko hayo, kwa sasa ramani zote za msingi na zile za mipango miji zimeingizwa kwenye mifumo ya kidigitali huku wamiliki wa ardhi wakianza kupokea bili za kodi ya pango la ardhi kupitia simu zao za kiganjani.

Nimshukuru sana Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiwezesha Wizara yangu kupata fedha za kufanikisha mageuzi makubwa yanayokwenda kuweka historia ndani ya sekta ya Ardhi na nchi kwa ujumla.

Niwatakie usomaji mwema wa Toleo hili Maalum.

**Mhe. Deogratius Ndejembi (Mb.)**
Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi.


## Bodi ya Wahariri

**MWENYEKITI**
Eng. Anthony Sanga

**MWENYEKITI MSAIDIZI**
Lucy D. Kabyemera

**MHARIRI**
Eleuteri Mangi

**WAANDISHI**
Munir Shemweta
Magreth Harrison
Goodluck Mwihava

**WAPIGA PICHA**
Manase Madelemu
Charles Mushi

**MSANIFU**
Joel Magese

# Salamu za Katibu Mkuu



Wiki ya Ardhi ni mkakati wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wa kuwakutanisha watumishi wa sekta ya Ardhi, wadau na wananchi kwa ujumla kujadiliana masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya ardhi zikiwemo changamoto na mbinu za utatuzi wa changamoto hizo.

Tukio hili linawaunganisha pamoja wataalam wa sekta ya Ardhi kwenye maeneo yote ya taaluma zao na taasisi zilizochini ya Wizara wakiwemo watumishi wa Ardhi katika Halmashauri na Makamishna wa Ardhi Wasaidizi ngazi ya mikoa wafanye kazi kwa pamoja ili kuwahudumia wananchi ipasavyo.

Washiriki katika Wiki ya Ardhi wamepata fursa ya kujiimarisha na kuhamasishana juu ya matumizi ya teknolojia kupitia mfumo mpya wa kidigitali wa e-Ardhi ambao umejengwa na wataalamu wetu wa ndani.

Mfumo huu ni utekelezaji wa maelekezo ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kuboresha utoaji wa huduma za ardhi, kuongeza uwazi na kuchochea maendeleo ya kijamii kidigitali kwa kujenga upya miundombinu na taasisi ili kufanyakazi kwa ufanisi.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imetafsiri dhana hiyo kwa kujenga mfumo wa e-Ardhi unaotumika kuweka na kutunza kumbukumbu zinazohusu masuala ya ardhi, kurahisisha kazi, taratibu za utoaji wa milki za ardhi, kuimarisha usalama wa milki za ardhi na kupata taarifa sahihi kwa wakati.

Hatua hii inasaidia kuimarisha upatikanaji wa huduma za ardhi kwa wananchi wetu kupitia mfumo wa kidigitali ambao umeboresha kasi ya upatikanaji wa huduma za ardhi kwa wakati, kutatua changamoto zilizopo katika sekta ya ardhi, kuharakisha utoaji wa huduma na kuhakikisha usimamizi bora wa rasilimali za ardhi.

Katika tafakari ya wiki hii, tunawasisitiza watumishi wote wa Wizara kujikita katika malengo mahususi ya wizara ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa uadilifu ili kutoa huduma stahiki kwa wananchi.

Nawakaribisha wasomaji wetu katika Toleo hili Maalum la Wiki ya Ardhi ili kupata taarifa za shughuli zilizofanyika ndani ya Wiki hii. Dhamira yetu ni kuifanya sekta ya Ardhi kuwa miongoni mwa sekta zinazochechemua uchumi wa taifa letu.

Karibuni sana

**Mhandisi Anthony Sanga**
Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

# Tumieni Mfumo wa e-ARDHI kikamilifu - Ndejembi



*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Deogratius Ndejembi akizungumza wakati wa ufunguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Ardhi yaliyofanyika tarehe 3 Desemba 2024 katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.*

Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Deogratius Ndejembi amewataka watendaji wa sekta ya ardhi nchini kuhakikisha wanatumia mfumo wa ardhi Kidigitali (e-Ardhi) kikamilifu kwa maeneo ambayo mfumo huo umeanza kutumika.

Mhe. Ndejembi alisema hayo wakati akizindua rasmi Maadhimisho ya Wiki ya Ardhi yaliyofanyika kuanzia tarehe 2 hadi 5 Desemba 2024 jijini Dodoma.

Kwa mujibu wa Mhe. Ndejembi, matumizi ya teknolojia siyo hiari kwa kuwa kupitia mfumo huo wa e-ardhi huduma za sekta ya ardhi zitaboreshwa na kuweza kuwafikia wananchi wengi wakiwemo wale wa vijijini.

Mfumo wa e-Ardhi tayari umeanza kutumika kwenye wmaeneo mbalimbali nchini kama vile Dodoma, Arusha, Tabora katika halmashauri ya Nzega, Pwani halmashauri ya Chalinze pamoja na manispaa ya Shinyanga na Kahama zilizopo mkoa wa Shinyanga.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii Mhe. Timotheo Mzava amesema baada ya Maadhimisho hayo ya Wiki ya Ardhi Bunge linatarajia sekta ya Ardhi itakuwa na mafanikio makubwa katika kuwahudumia wananchi ikizingatiwa kuwa, watumishi wa Sekta ya Ardhi wanaoshiriki maadhimisho



hayo wanatoka katika mikoa na halmashauri zote nchini.

Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi inaadhimisha Wiki ya Ardhi kuanzia tarehe 2 hadi 5 Desemba 2024 ambapo mbali mambo mengine wiki hiyo inatumika kujadili utoaji huduma za kisekta pamoja na uwepo mawasilisho mbalimbali kwa lengo la kufanya maboresho ya maeneo yenye changamoto.

# Pinda ahimiza utoaji wa hati kwa wakati




*Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Geophrey Pinda akizungumza wakati wa kufunga Maadhimisho ya Wiki ya Ardhi tarehe 5 Desemba 2024 katika viwanja vya Ukumbi wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma.*

Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Geophrey Pinda amewahimiza Wasajili wa Hati na Nyaraka Wasaidizi katika ofisi za Ardhi za Mikoa kuhakikisha wanatoa Hati Milki za Ardhi kwa wakati kwa wananchi walioomba kupatiwa hati hizo.

Mhe Pinda ametoa kauli hiyo Desemba 5, 2024 wakati wa kufunga Maadhimisho ya Wiki ya Ardhi jijini Dodoma na kuwasisitiza wasajili wa Hati kutoa hati kwa wakati ili kutoikosesha serikali mapato yatokanayo na kodi ya ardhi.

“*Wasajili wa Hati wanapataje afua kama mwananchi anasumbuliwa kupata Hati Milki ya Ardhi kwa mwaka mmoja au miezi sita wakati angeweza kupata hati ndani ya wiki moja*” amesema Mhe. Pinda.

Aidha, Mhe. Pinda amewapongeza watumishi wa sekta ya ardhi kwa kushiriki katika mageuzi makubwa ya wizara hiyo ambapo sasa wizara ya ardhi imeingia kwenye mfumo wa kidigitali (e-ardhi) jambo alilolieleza linalenga kuboresha huduma za sekta hiyo.

Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi inaadhimisha Wiki ya Ardhi kuanzia tarehe 2 hadi 5 Desemba 2024 ambapo mbali mambo mengine wiki hiyo inatumika kujadili utoaji huduma za kisekta pamoja na uwepo mawasilisho mbalimbali kwa lengo la kufanya maboresho ya maeneo yenye changamoto.

# Mhandisi Sanga aagiza kufanya vikao kabla ya kazi

Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhandisi Anthony Sanga ameziagiza ofisi zote za Ardhi nchini kuanzia mkoa hadi halmashauri kuhakikisha zinakaa vikao vya muda mfupi kila asubuhi kabla ya kuanza kazi ili kuwa na njia bora ya kutatua changamoto za sekta hiyo.

Amesema, utaratibu wa kuwa na vikao vya muda mfupi kila siku asubuhi kutawawezesha watendaji wa sekta ya ardhi nchini kujua namna ya kushughulika na changamoto zinazojitokeza mara kwa mara katika maeneo yao ya kazi.

"Mnapokutana mnakaa kwanza vikao vifupi kila subuhi kabla ya kuanza kazi na kupanga mipango, hata kama kikao cha cha dakika tano ili kuona jana mlifanya kazi vipi na kuna changamoto gani ili mzishughulikie" amesema Mhandisi Sanga.



*Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhandisi Anthony Sanga akizungumza na watumishi wa Ardhi katika Maadhimisho ya Wiki ya Ardhi yaliyofanyika tarehe 2 hadi 5 Desemba 2024 katika Viwanja vya Ukumbi wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma.*

Katibu Mkuu Mhandisi Sanga ametoa maagizo hayo tarehe 2 Desemba 2024 katika ukumbi wa Jakaya Kikwete wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Ardhi yaliyofanyika jijini Dodoma.

Aidha, amewataka watendaji wa sekta ya Ardhi nchini kujitambua na kuelewa kuwa, watumishi wote wa sekta hiyo ni wamoja na wananchi wanaelewa kuwa wote ni watumishi wa Ardhi bila kuchanganua taaluma zao.

"Unapomuambia mwananchi ramani haijapanda yeye haelewi , usimtume mwananchi bali wewe msaidie, masuala ya ramani ni masuala yenu ya kitaaluma na tutoke katika tabia hiyo na kwenda kusaidia wananchi" amesema Mhandisi Sanga.



Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi SMZ Bi Mhaza Gharib Juma amesema, Wiki ya Ardhi inayoadhimishwa itaimarisha mashirikiano baina ya Zanzibar na Tanzania Bara katika masuala ya sekta ya ardhi hasa ikizingaitiwa lengo kuu la serikali zote mbili ni kuisaidia jamiii.

Aidha, ametaka kuangaliwa namna sekta ya ardhi itakavyoimarisha masuala ya uwekezaji sambamba na ardhi kutumika kwa uadilifu na haki ili kuimarisha uwekezaji na kupata fedha zitakazowezesha upatikanaji huduma mbalimbali.

# Hakikisheni thamani halisi ya Ardhi inajulikana

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Deogratius Ndejembi amewataka Wathamini nchini kupunguza migogoro inayotokana na uthamini kwa kuhakikisha thamani halisi ya ardhi inayofanyiwa uthamini inajulikana.

Mhe. Ndejembi amesema hayo kwenye Mkutano Mkuu wa Bodi ya Usajili wa Wathamini (VRB) ambao ni sehemu ya Maadhimisho ya Wiki ya Ardhi 2024 yaliyoandaliwa na wizara kwa mara ya kwanza nakufanyika kuanzia Desemba 2 hadi 5, 2024 jijini Dodoma.

Amesema, teknolojia inabadilika katika nyanja mbalimbali ikiwemo njia ya mawasiliano, namna ya kufanya kazi na biashara ambapo ameweka wazi kuwa, taaluma ya uthamini nayo haiko nyuma na inapaswa kuendana na mabadiliko hayo.

“Kama wathamini, ni muhimu mjikite katika matumizi ya zana za kidijitali zinazopatikana kwenu, kutoka kwa mifumo ya Kijiografia (GIS), Akili Bandia (AI), na Mifumo mbalimbali ya kidijitali. Teknolojia hizi zinawapa uwezo wa kufanya uthamini za ardhi na mali kwa usahihi zaidi na kwa ufanisi zaidi” amesema Waziri Ndejembi.

Waziri Ndejembi amewataka wathamini kuunganisha



teknolojia katika kazi zao za kila siku kwa kuwa kunaboresha usahihi wa kazi za uthamini sambamba na kuimarisha uaminifu wa taaluma hiyo ili kukuza uwazi na haki, jambo ambalo alilolieleza linajenga imani miongoni mwa wawekezaji, taasisi za serikali, na jamii kwa ujumla.

“Hivyo, nawaasa kila mmoja wenu kujitahidi kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia, kuwekeza katika maendeleo yenu ya kitaaluma na majukwaa mbalimbali ya kidijitali ambayo yanaweza kuboresha kazi zenu” amesema Waziri Ndejembi.

Kwa upande wake, Msajili wa Bodi ya Wathamini nchini Bw. Joseph Shewiyo amesema, kwa sasa kuna zaidi ya Wathamini 400 nchini ambapo kupitia mahafali hayo jumla ya wahitimu 34 wamehitimu.

Mkutano huo wa mwaka wa Bodi ya Usajili wa Uthamini (VRB) unaongozwa na Kaulimbiu “Mwelekeo wa Uthamini Tanzania; Kujumuisha Teknolojia, Uvumbuzi na Ustahimilivu wa Mazingira” kaulimbiu inayohimiza kuendelea kuzingatia mabadiliko ya kimataifa na maendeleo ya kiteknolojia kwa kuzingatia umuhimu wa uendelevu na ustahimilivu wa mazingira.

# Wataalamu Mipango Miji wakutana Dodoma Kuweka Mikakati





Wataakamu wa Mipangomiji nchini wamekutana na kuweka mikakati yenye tija ya kuwahudumia wananchi. Wataalamu hao wamekutana kwenye mkutano mkuu wa tisa wa Mwaka wa Maofisa Mipangomiji Tanzania Bara ulioenda sambamba na Maadhimisho ya Wiki ya Ardhi yaliyofanyika kuanzia tarehe 2 hadi 5 Desemba 2024 jijini Dodoma.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Msajili wa Bodi ya Usajili wa Wataalamu wa Mipangomiji (TPRB) Lucas Mwaisaka, amesema, kupitia mkutano huo wataalamu hao wamefanya tathmini na kubadilishana uzoefu katika utendaji kazi wao ili kuondokana na changamoto ya makazi holela kwenye maeneo mbalimbali nchini.

“Tumejadili namna ya kutumia teknolojia kusimamia shughuli zote za Mipangomiji, tumefanya kazi kubwa ya kuanzisha mfumo ambao umeunganishwa na e-Ardhi ili kudhibiti na kufanya kazi kwa haraka kuwahudumia wananchi kupitia mifumo,”anasema.

Kwa mujibu wa Mwaisaka, bodi yake tangu ianze kufanya kazi Mwaka 2009 imesajili kampuni 101 na wataalamu 546 huku kampuni 11 na wataalamu 32 wakifutiwa usajili kutokana na kukiuka Sheria ya Mipangomiji katika utekelezaji majukumu yao.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Mipango na Matumizi ya Ardhi (NLUPC), Bw. Joseph Mafuru, anasema upimaji na upangaji shirikishi kwa wananchi kwenye mitaa na vijiji ndiyo mwarobaini wa kuondokana na wimbi la ubadilishaji wa matumizi ya ardhi iliyopangwa.

Ameweka wazi kuwa, ramani za mipangomiji zinapaswa kuonesha maeneo yalivyopangwa, matumizi ya ardhi husika ikiwemo makazi, biashara, viwanja vya michezo, maeneo ya kupumzikia, shule, hospitali na huduma zingine za msingi jambo alilolieleza kuwa, linawasaidia wananchi kujua matumizi ya maeneo yao na kuyalinda kwenye mitaa yao.

Bodi ya Usajili wa Wataalamu wa Mipangomiji nchini (TPRB) ni taasisi ambayo iko chini ya Wizara ya Ardhi yenye lengo la kuwa na taaluma iliyojidhatiti miongoni mwa wataalamu na makampuni yanayotoa huduma za upangaji wa miji sambamba na kuboresha viwango na ubora wa mipango miji katika nchi.

Jamhuri ya
Muungano wa
Tanzania

Wizara ya Ardhi
Nyumba na Maendeleo
ya Makazi

# Lipa Kodi


## ya Pango la Ardhi

Jinsi ya kujua kiasi unachodaiwa na namna ya kulipa

## Piga *152*00#

Kisha Chagua 1. Malipo

2. Kadiria Kodi ya Kiwanja
3. Chagua 1: DAR au 2 kwa viwanja vingine.
4. Chagua 1 kwa kutumia Namba ya Hati au 2 kwa kutumia ID namba (Lot ID).
5. Bonyeza TUMA
6. Subiri namba ya Malipo ( control number ) inayoanzia na 99117... na kiasi unachotakiwa kulipa.
7. Tumia namba ya Malipo na Kiasi ulichotumiwa kufanya malipo kwa kupitia mitandao ya simu na Benki.




www.lands.go.tz

@wizara_ya_ardhi/Ardhi TV

# Kutana na Mpima wa kwanza Mwanamke Tanzania




Bi. Nina Nimwesigwa Rutakyamirwa, Mpima wa kwanza mwanamke Tanzania ambaye kwa sasa ni mwajiriwa wa Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi akihudumu ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi mkoa wa Pwani.

Nina alihitimu mafunzo yake mwaka 1992 katika Chuo Kikuu cha Ardhi na kupata ajira ya moja kwa moja kwa maelekezo ya aliyekuwa Rais wa Serikali ya Awamu ya Pili Hayati Ally Hassan Mwinyi.

“Namshukuru Mungu kwamba wakati namaliza chuo mgeni rasmi alikuwa Rais wa Serikali ya Awamu ya Pili Hayati Ally Hassan Mwinyi alinipa ajira ya moja kwa moja” anasema Nina. Mpima huyo wa kwanza mwanamke ameelezea mapito yake hadi kuwa mtaalamu wa fani ya upimaji ambapo amesema haikuwa kazi rahisi kutokana na changamoto kadhaa alizozipitia.

Kwa mujibu wa Nina, alisomea fani ya Upimaji Ardhi kwa kutiwa moyo na kaka yake sambamba na walimu wa chuo ingawa wakati mwingine alikatishwa tamaa kwa kuelezwa kuwa ameingia katika fani ya wanaume.

Amesema, pamoja na changamoto mbalimbali lakini hakukata tamaa katika kufanikisha lengo lake jambo alilolieleza limefanya afanikiwe azma yake na hatimaye kuwa mpima wa kwanza mwanamke Tanzania.

“Kuna wakati tulipoenda field, kwa sababu nilikuwa na wanaume wakasema nitakuwa mpishi wao, na niwe mkweli niliwakatalia na kuwaeleza nimekuja kujifunza kama ninyi” amesema.

Nina anaeleza kuwa, anajivunia kushiriki kazi mbalimbali ikiwemo miradi ya upimaji mashamba na mipaka ya vijiji katika maeneo mbalimbali nchini jambo alilolieleza linampa faraja sana.

Ametoa wito kwa wapima ardhi wanawake nchini kufanya kazi kwa bidii na kutokata tamaa huku akiwaasa wanaochukua fani hiyo kusoma kwa bidii na kujikita zaidi katika mafunzo ya vitendo badala ya kusoma kwa kufaulu mitihani.

Huyo ni Nina Nimwesigwa Rutakyamirwa, Mpima wa kwanza Mwanamke Tanzania.

# Wapima Ardhi Wapigwa Msasa

Wapima Ardhi waliohudhuria mkutano mkuu wa mwaka wa Taasisi ya Wapima Ardhi Tanzania (IST) wamepata mafunzo kuhusu mfumo wa e-ardhi ili kuboresha utendaji kazi wao.

Katika mkutano wao uliofanyika jijini Dodoma wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Ardhi tarehe 4 Desemba 2024 mawasilisho mbalimbali yalitolewa kwa lengo la kuwajengea uwezo wataalamu hao ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na haraka katika maeneo yao.

Akizungumza na Jarida Maalumu la Ardhi Yetu, Mwenyekiti wa Bodi ya Wapima Ardhi nchini na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Hamdouny Mansoor anasema, tuna jukwaa letu la wapima Tanzania ambalo linawakutanisha Wapima wote, waliopo katika majukumu ya kiserikali, makampuni pamoja na wale wapima wote waliosajiliwa".

Akielezea utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya bodi hiyo ya wapima, Mansoor anasema, bodi yake imeshughulikia jumla ya maombi 55 ya Wapima wa kudumu, wapima wa awali pamoja na maombi ya kutoa leseni za makampuni ili yaweze kufanya kazi ya Upimaji.



Kwa upande wake Rais wa Taasisi ya Wapima Ardhi nchini (IST) Dkt. Julian ulian Magenzi anasema Wiki ya Ardhi ina manufaa makubwa kwa Wapima Ardhi kwa kuwa imeongeza tija kwa kuwajengea uwezo kwa kujifunza kutokana na mawasilisho mbalimbali na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

"Kutokana na mabadiliko ya Teknolojia, taaluma ya Upima Ardhi imekuwa na mabadiliko mbalimbali ambayo yamesaidia kuboresha vitendeoa kazi hatua inayosaidia kupunguza gharama za upimaji na utendaji kazi wa haraka kutokana na Teknolojia hizo". amesema.

Kikao cha Taasisi ya Wapima Ardhi Tanzania (IST) hufanyika kila mwaka kwa kuwakutanisha Wapima Ardhi wote nchini kwa lengo la kuangalia mambo yanayohusu taaluma hiyo na changamoto zake ili kuzitafutia ufumbuzi na kwa mwaka huu taasisi hiyo ya wapima imetimiza miaka 42.

# Burudani

Mziki

# kazi na dawa, burudani ndani ya Wiki ya Ardhi



*Msanii wa Mziki Peter Msechu akiimba pamoja na watumishi wa wizra ya ardhi wakati wa ufunguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Ardhi yaliyofanyika tarehe 3 Desemba 2024 katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.*

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeanzisha mkakati wa kukutana na watumishi na wadau wa Sekta ya Ardhi nchi nzima kubadilishana uzoefu ili kutoa huduma bora na stahiki kwa wananchi kwa wakati.

Wiki ya Ardhi ni mkakati ulioanzishwa na wizara kwa lengo la kuwaleta pamoja wadau wa sekta ya ardhi nchi nzima kuanzia ngazi makao makuu hadi halmashauri zote Tanzania Bara ili kujadiliana na kuona namna bora ya kuboresha utendaji kazi utakaoenda sambamba na utoaji huduma bora kwa wananchi.

Wajihi wa Wiki ya Ardhi unapambwa kwa huduma mbalimbali za ardhi na kuchagizwa kwa burudani na mirindimo kutoka kwa wasanii Peter Msechu, Kikundi cha Ngoma cha Mchoya kutoka Wilaya ya Chamwino na msanii Mary kutoka Taasisi ya Kuzuia na kupambana na Rushwa nchini (PCCB).

Usemi wa kazi na dawa, unadhihirishwa na Wataalamu wa sekta ya Ardhi waliosakata muziki wenye ujumbe wa kuhamasisha hadhira kumiliki na kutunza ardhi wakiongozwa na Msanii Msechu kwa wimbo wake maridhawa 'Ardhi ni Mtaji Itunze Ikutunze'.

Maadhimisho haya ya Wiki ya Ardhi ambayo yamefanyika kwa mara ya kwanza mwaka huu wa 2024 yanawaunganisha Watumishi Serikali sekta ya ardhi na wadau ili waendelee kuwa daraja moja la kuwahudumia Watanzania na wawekezaji kwenye sekta mtambuka ya ardhi.

Hatua hii ya wizara inaunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Jemedari Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa maendeleo endelevu, 'Kazi Iendelee'.

# HABARI PICHA KATIKA MAADHIMISHO YA WIKI YA ARDHI






JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI
MAADHIMISHO YA WIKI YA ARDHI
KAULI MBIU: "Ardhi Kidigitali, Ufanisi katika Upatikanaji wa Huduma kwa Wananch
2 - 5 DESEMBA 2024
UKUMBI WA MIKUTANO WA JAKAYA
KIKWETE DODOMA
MHE. DEOGRATIUS NDEJEMBI


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI
MAADHIMISHO YA WIKI YA ARDHI


JAMH
WIZARA YA AR
MAADHIM


KAULI MBIU: "Ardhi Kidigitali, Ufanis
2 - 5 DESEMB 2024
UK
KIK
MGE
Waz













# Mawasiliano

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

S.L.P 2908 DODOMA

Instagram: @wizara_ya_ardhi

Tovuti: www.lands.go.tz

Baruapepe: ps@lands.go.tz